



**MASENO UNIVERSITY**  
**UNIVERSITY EXAMINATIONS 2013/2014**

FOURTH YEAR FIRST SEMESTER EXAMINATIONS FOR THE  
DEGREE OF BACHELOR OF ARTS AND BACHELOR OF  
EDUCATION WITH INFORMATION TECHNOLOGY  
(MAIN CAMPUS)

**AKI 405: DISCOURSE ANALYSIS**

---

*Date: 28<sup>th</sup> November, 2013*

*Time: 8.30 - 10.30 a.m.*

---

CHUO KIKUU CHA MASENO

(*Main Campus*)

KOZI: AKI 405 DISCOURSE ANALYSIS (UCHANGANUZI WA USEMI)

MAAGIZO: JIBU SWALI LA KWANZA NA MASWALI MENGINE MAWILI.

MUDA: SAA 2

S1. Changanua mshikamano katika matini yafuatayo. (*Alama 26*)

Kabla ya kuasi, Shetani alikuwa katika hadhara takatifu. Baada ya kuasi, shetani kawa Rajimi. Ikiwa tunathubutu kuitazama nidhamu ya hadhara takatifu kuwa ni nidhamu ya 'kisiasa' basi pengine tungaliweza kumwita Ibilisi 'mtimba-kwiri' na labda maana hiyo ingalikuwa maana iliyo karibu zaidi na Rajimi katika maisha ya kisasa. Kwa upande wa pili miwenye Inkishafi anasema moyo wake umetwaliwa na mapenzi ya ulimwengu. Hili tulifafanuwe vipi? Kwa Wakristo, vivyo kwa Waislamu, mapenzi ya ulimwengu ni moja kati ya maasi. Na hoja inayotolewa ni hii. Ulimwengu umeumbwa kama njia alivyoumbwa. Kwa hivyo kila njia 'anavyoupupia' (nikitumia msamiati wa Biblia) basi ndivyo anavyozidi kuwa mbali na aliyemuumba. Msano wenyewe ni kama mtu aliyekuwa yupo baina ya vituo viwili kimoja ni Dunia na cha pili ni Mola. Basi kila akiwa anakaribia kimoja, anazidi kuwa mbali na cha pili. Msanifu wa Inkishafi yuko baina ya maovu mawili 'mapenzi ya dunia' na Vitimbi<sup>1</sup> vya Ibilisi: kazingiwa kote kote 'mzingile mwanambiji' kama marehemu Kaluta Amri Abeid angaliuuta. Katika Biblia, kwenye Chuo cha Warumi tunaasoma: 'Dunia isipige zumari, mkainuka na kuchenza' (tafsiri yangu) na katika hadithi ya Mtume (SAW) tunaambiwa: mapenzi ya dunia - ndio shina la maovu yote. Kunga anayotumia msanii hapa kwenye mstari huu anaposema moyo wake 'utetwe ni hawaa ya ulimwengu' ni kunga ya tash-khis. Yaani ile kunga ya kukijaalia kitu kisicho na roho au kisicho sifa za binadamu, sifa hizo. Msanii anayazungumza mapenzi ya ulimwengu kama yenyе mikono na uhai. Yanaweza kutwaa. Yanaweza kutupa. Nasema kunga ya tash-khis. Yaani kunga ya kukijaalia kitu sifa za mwanadamu si kiroja katika fasih ya Kiswahili kama ilivyokuwa si kiroja katika fasih ama methali za lugha nyenginezo. Hebu tunrejee marehemu Sheikh Shaaban Robert katika kitabu chake cha *Maisha ya Sit* anaposema: 'Dunia imezoweya kuwa popu ya kuona bidii na matendo mazuri ya watoto wake wakati wa maisha yao ya mwili. Katika giza la sahau kuu ndipo ilipozindukana katika usingizi wake mzito, ikajaribu kuokota na kuunga pamoja viungo vya mkufu wa maisha 'bora'. Dunia hapo imefanywa kama mwanadamu; kama 'hawaa ya ulimwengu' kwenye ubeti huo wa Inkishafi.

(Muhamadi wa Mlamali, 1980:13)

- S2. Fafanua mielekeo mbalimbali ya taaluma ya uchanganuzi wa usemi. (Alama 22)
- S3. Dhihirisha jinsi kaida za **Kanuni ya Ushirika** (Grice, 1975) zinavyoweza kuendelezwa na kukiukwa katika mazungumzo. (Alama 22)
- S4. Fafanua nadharia ya **Tukio Kauli** katika muktadha wa arusi. (Alama 22)
- S5. Huku ukitoa mifano faafu eleza misingi ya nadharia ya **Tendo Kauli**. (Alama, 22)
- S6. Onyesha jinsi mfuatano rudufu wa ushikaji zamu unavyodhiihika katika mazungumzo. (Alama22)

Maseno University



ISO 9001: 2008 Certified